

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA SITINI NA MBILI

30 JUNI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA SITINI NA MBILI – TAREHE 30 JUNI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2021*].

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2021*].

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**519. MHESHIMIWA JOSEPH KASHEKU
MUSUKUMA (GEITA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya Kidato cha Tano na Sita katika Shule ya Sekondari Bugando iliyopo Tarafa ya Bugando na Shule ya Sekondari ya Rubanga iliyopo Tarafa ya Isulwabutundwe.

**520. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO
MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Ujenzi wa Barabara za Kwasadala – Jiweni, Mashua - Shirinjoro – Mijongweni, Kalali – Nronga, Arusha Road – Mlimashabaha – Sanya Statesheni pamoja na Kwasadala – Uswaa.

**521. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE
(NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itasaidia na kufanikisha kutoa namba kwa Vijiji vya Chipunda Kata ya Namatutwe, Mkalinga Kata ya Chikunja na Sululu ya Leo Kata ya Namatutwe vyenye Wakazi zaidi ya elfu kumi katika Jimbo la Ndanda.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI:**

**522. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI
CHAUREMBO (MBAGALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyarudisha kwa Halmashauri maeneo yote yasiyoendelezwa na Mashirika ya Umma kwa zaidi ya miaka kumi ili Halmashauri zijenge Miundombinu ya huduma za Jamii.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

523. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE (KILWA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Barabara ya Nangurukuru – Liwale yenye Kilomita 258 itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kama Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025 inavyoelekeza.

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

524. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuhamisha Dawati la Kijinsia kutoka Jeshi la Polisi na kwenda kwenye Vituo vya kutolea Huduma za Afya.

WIZARA YA NISHATI:

525. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itawasha umeme kwenye Vijiji na Vitongoji vyote katika Jimbo la Arumeru Mashariki ambavyo umeme bado haujawashwa.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

526. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi imebana sana maeneo ya Wananchi na kusababisha kazi za Kijamii katika Kata za Lunguza, Mng'aro na Mnazi kushindwa kufanyika:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kupunguza sehemu ya Hifadhi ya Mkomazi na kugawa kwa Serikali za Vijiji.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

527. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS SAID GULAMALI (MANONGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa Majosho katika Wilaya ya Igunga hususan Jimbo la Manonga.

WIZARA YA MAJI:

528. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza vituo vya kuchotea maji katika Mji Mdogo wa Gairo.

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2021*].

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani wa Mwaka 2021 [*The Road Traffic (Amendment) Bill, 2021*].

V. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2021*].

VI. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:

VII. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:

WAZIRI MKUU:

VIII. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI:

**DODOMA
30 JUNI, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**